OFISI YA RAISI-TAMISEMI

MKOA WA MWANZA

SHULE YA SEKONDARI MWAMASHIMBA.

S.L.P 66,

NGUDU/KWIMBA.

Kumb.Na.MWASS/MK/VOL…….. TAREHE……/……/……

SIMU:

1. MKUU WA SHULE: ***0765 622 601***
2. MAKAMU MKUU WA SHULE: ***0752 066 602 / 0789 013 375***
3. MATRON: ***0764 565 561 / 0746 651 903***

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA TANO……
KATIKA SHULE YA SEKONDARI MWAMASHIMBA.

Ninayo furaha kukupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na kidato cha TANO katika shule ya sekondari Mwamashimba iliyoko wilayani Kwimba,Mkoa wa Mwanza.

1.MAHALI SHULE ILIPO.

Shule ya sekondari mwamashimba imo ndani ya kijiji cha Sanga,Kata ya Fukalo,Tarafa ya Mwamashimba.Ipo umbali wa kilomita 61 kutoka makao makuu ya wilaya ya kwimba na kilomita 20 tu kutoka barabara kuu ya Mwanza-Shinyanga mwendo wa dakika 20 tu kutoka kituo cha Hungumalwa.Ukitoka Mwanza, utapanda magari ya katika stend kuu ya Nyegezi-Magari yaendayo shilima.Ukitoka Shinyanga, shuka kituo cha Mabasi Hungumalwa na subiri mabasi yatokayo mwaza ambayo hufika hapo kuanzia saa sita mchana.

KUFUNGUA SHULE.

Shule itafunguliwa tarehe……. na masomo yataanza mara moja.

2.Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare ya shule

a) Sare ya shule hii ni sketi 2 za rangi ya zambarau(purple) zenye marinda ya kufuatana yenye upana wan nchi 2.5 urefu ivuke magoti kwa nchi 8 au zaidi.(*kipande cha kitambaa na picha ya mshono vimeamatanishwa*)
b) Rangi ya hijab au nusu kanzu ni nyeupe na ushungi mweupe.
c) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba na vyenye visigino vifupi.
d) Soksi jozi mbili nyeupe (stocking)
e) Sweta ya blue isiyo na michirizi iwe na nembo ya shule
f) Tai ndefu yenye rangi ya zambarau (kitambaa cha sketi ya shule)
g) Nguo za kushindia, sketi moja nyeusi yenye marinda ya kufuatana yenye upana wa nchi 2.5 na urefu ivuke magoti kwa nchi 8 au zaidi.
h) T-shirt nyekundu isiyo na kola iwe na nembo ya shule
i) Sare ya michezo ni Tracksuit ya rangi ya Blue
j) Raba nyeusi jozi moja kwa ajili ya michezo

2.2. Ada na michango ya shule

a) Ada ya shule kwa mwaka ni shillingi elfu sabini (70,000/=) kwa mwanafunzi wa bweni.Unaweza kiasi cha shilingi 35,000/= kwa nusu muhula au ada yote kwa mara moja.Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule namba. **3151100456** katika Benki ya NMB tawi lolote lililopo karibu nawe (*Tafadhali andika Jina la mwanafunzi kwenye pay in slip*)

b) Mchango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-
   i. Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani.
   ii. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha(Aje na fedha taslimu/cash).
   iii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya Taaluma.
   iv. Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi,walinzi na vibarua wengine.
   v. Shilingi 2,000/= kwa ajili ya nembo ya shule.
   vi. Shilingi 5,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza.
   vii. Shilingi 5,000/= kwa ajili ya C.H.F kwa wanafunzi wasiokuwa na Bima(Aje na fedha taslimu/cash).
   viii. Shilingi 20,000/= Mitihani ya kujipima (mock) kidato cha sita(Ilipwe akiwa kidato cha sita).
   ix. Fedha ya tahadhari 5,000/= (haitarejeshwa).

c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni ni:-

i. Ream ya karatasi 1 (Kwa mwaka).
ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
iii. Scientific calculator, kwa wanafunzi wanaosoma Geography
iv. Godoro kwa wanafunzi wa bweni (size 3*6)
v. Mashuka 2 (lightblue), foronya 2 (rangi ya light blue), mto mmoja (1), na chandarua 1 (lightblue).
vi. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe).
vii. Dumu dogo Lita 5 kwa ajili ya maji ya kunywa.
viii. Ndoo mbili kubwa zenye mifuniko.
ix. Taulo 1, Night dress 1, hanger 1 (plastic) ya kuanikia nguo za ndani.
x. Kwanja 1(kwa HKL), jembe 1na mpini(HKL,HGL na HGK), Reki 1 yenye mpini(HGK).
xi. Fagio ya ndani (softbloom) Kwa HGL tu.
xii. Fagio ya nje (chelewa ndefu) Michepuo yote.
xiii. Folder file ndogo 1.
xiv. Counter books(quire 3), Yasipungue madaftari saba(7)

3.MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi,kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule.
vi. Kusuka. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
viii. Uvutaji wa sigara.
ix. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xi. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xiii. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

xiv. Kudharau Bendera ya Taifa.
xv. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua, kama kunywa sumu n.k.
xvi. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

4.Viambatisho na fomu muhimu.

1) ***Kiambatisho A***: Fomu ya uchunguzi wa Afya (medical examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali.
2) ***Kiambatisho B:*** Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
3) Picha mbili (2) za Wazazi au Ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

Saini ya Mkuu wa Shule……..

Jina la Mkuu wa Shule……

Mhuri wa Mkuu wa Shule……

KWIMBA DISTRICT COUNCIL *Kiambatisho A*

MWAMASHIMBA SECONDARY SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM

(To be completed by the medical Officer in respect of all form five students).

PUPIL'S FULL NAME:…….

AGE…….....YEARS. SEX…….

STOOL EXAMINATION:……

BLOOD COUNT (RED AND WHITE):…….

URINALYSIS……

SYPHILYSIS TEST…….

T.B. TEST:……

CHEST:……

SPLEEN:……

ABNORMAL INFORMATION. e.g. Physical defects, impairment, chronic or Family diseases etc.

……
……
……
……

I certify that I have examined the above student and recommend that She is fit/unfit to pursue further education.

Signature……..

Designation……

Date……. Official stamp.……

(Delete whichever is inapplicable)

SHULE YA SEKONDARI MWAMASHIMBA ***Kiambatisho B***

MAELEZO KUHUSU HISTORIA NA MAKAZI YA MWANAFUNZI AWAPO SHULENI/MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO,FUJO NA MAKOSA YA JINAI.

A.MAELEZO BINAFSI.

1. ina la mwanafunzi…….. Kidato cha…… Jinsia (me/ke)
2. abila…….. Dini……..
   Tarehe ya kuzaliwa……/……/…….. Uraia……

B.WAZAZI/WALEZI

1. ina la baba…… Je yupo hai? (NDIYO/HAPANA)
2. ina la mama…… Je yupo hai? (NDIYO/HAPANA)
3. ama baba na mama wamefariki/wanaishi mbali:-
   a) ina la mlezi wako……
      Uhusiano wake na mlezi ni (mjomba, shangazi, Baba mdogo. n.k)
   b) azi ya baba/ mlezi……..
      Eneo la kazi /idara……
   c) azi ya mama…….. Eneo la kazi/idara……
      Wote wazazi wako wanaishi pamoja/wametengana?……..

C. MAKAZI YA WAZAZI/WALEZI

a. aba…….. Wilaya…… Kitongoji……
   Mtaa…….. Namba ya Nyumba……..
b. ama…….. Wilaya…… Kitongoji……
   Simu…… / …… /……. (Baba)

……/ ……/…… (Mama)
……/ ……/ …… (Mlezi)

D. Mimi ……..(Jina la mwanafunzi) naahidi kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa yoyote ya jinai.